JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

Juni, 2023

Dodoma

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu 0752306858**

**Mkuu wa Shule 0719407373**

**Makamu Mkuu wa Shule 0628200625**

**Patron 0752017239**

**Shule ya Sekondari Msamala**

**S.L.P. 599**

**Tarehe 12/06/2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ............**
**..................................................**
**S.L.P ...........................................**
**..................................................**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MSAMALA HALMASHAURI YA MANISPAA SONGEA MKOA WA RUVUMA MWAKA 2023/2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023/2024 na atasoma tahasusi ya ............

Shule ya Sekondari Msamala ipo umbali wa Kilometa 6 Kaskazini mwa Mji wa Songea. Usafiri wa basi kutoka kituo kikuu cha mabasi cha **Shule ya Tanga** unapatikana kwa Nauli ni Shilingi 700/= (Dala dala) kuelekea Mjini. Shuka kituo kiitwacho **OTTAWA.** Hapo pana usafiri wa pikipiki kwa Shilingi 1,000/=.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 14/08/2023 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/08/2023 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/08/2023

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni Esteem namba 9. Mshono wa suruali iwe yenye marinda matatu (3) pamoja na upana wa size 16 chini.
ii. Mashati meupe mawili (2) yenye mikono mirefu.
iii. Sare ya Michezo ni truck suit ya Blue Bahari pamoja na bukta na fulana yenye rangi yoyote.
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeusi za shule;
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
vii. Sweta bluu iliyoiva yenye shingo la V mbele.
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) Suruali rangi ya dark bluu mshono kama maelekezo namba (i)
ix. Tai yenye rangi ya suruali ya sare ikiwa na alama V (alama V iwe rangi ya kijani)
x. Tisheti rangi ya dark bluu yenye kola.

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari ya kutosha kwa masomo husika.
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
iv. Scientific Calculator;
v. Mashuka Jozi 2, rangi ya bluu bahari, blanket 1, godoro 1 na foronya yake, chandarua 1 rangi yoyote.
vi. Nguo za ndani za kutosha;
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
ix. Kwanja 1, jembe 1, mopa 1, hard broom 1 na soft broom 1.

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**b) Shule za Kutwa**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 35,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **50,000/=** |

Michango yote iwekwe kwenye **namba 61801200088 NMB**. Jina la akaunti ni shule ya sekondari Msamala

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kufuga ndevu;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

x. Kusababisha mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule** ...........................................

**Jina la Mkuu wa Shule; Godfrey Ponera**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule** ...................................

HEADMASTER
MSAMALA SECONDARY SCHOOL
Box 599-SONGEA

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI**

**UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0719407373**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0628200625.**
- **Mwandamizi Taaluma 0767193433**
- **Mwandamizi Malezi 0755169677**

KIAMBATISHO A

MEDICAL EXAMINATION FORM

SONGEA MUNICIPAL COUNCIL

MSAMALA SECONDARY
SCHOOL
P. O. BOX 599
SONGEA

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please examine
Mr/Miss…………………………………………………………………………………………. as to his/her physical and mental fitness for admission as a form FIVE student for the Academic year 2023/2024.

Your sincerely,

……………………………………………………
THE HEADMASTER

HEADMASTER
MSAMALA SECONDARY SCHOOL
Box 599-SONGEA

The Headmaster, I have examined
Mr./Miss………………………………………………………………….as shown below and consider that he/she is physically and mentally fit/unfit for admission to pursue a full time secondary school education.

1. Vision with/without glasses: Right……………………………… Left…………………
2. Blood pressure…………………………………………….Hemoglobin……………………………
3. Hearing………………………………………………………………………………………
4. (a) Urine Albumen…………………………………… (b) Sugar………………………………
5. (a) Venereal diseases……………………………….. (b) Bilharzias………………………
6. Pregnancy……………………………………………………………………………
7. Neurosis………………………………………………………………………………
8. Is there any abnormality of;-
   (a) The heart……………………………………… (c) The spleen………………
   (b) Lungs……………………………………………………………………….
9. Are there any serious disease e.g. Leprosy, Asthma, Diabetes, etc.

   ……………………………………………………………………………………………………

   Date:…………………………………Station;…………………………………………………

   ……………………………

   Signature of Medical Officer Designation ………………

KIAMBATISHO B

## KUMBUKUMBU MUHIMU ZA MWANAFUNZI

1. Jina la Mwanafunzi ;……………………………………………………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa; ……………………………………………Mahali; …………………
3. Jina la Baba/Mlezi;……………………………………………………Hai/amefariki;………
4. Mahali anapoishi; Kijiji/Mji………………………… ... Wilaya……………..........
   Mkoa……………
5. Kazi ya Baba/Mlezi………………………………………………………………………
6. Namba yake ya simu; ………………………………………………………………………
7. Jina la Mama/Mlezi; ………………………………………………………………………
8. Mahali anapoishi;
   Kijiji/Mji………………………………Wilaya…………………………………Mkoa…..
9. Kazi ya Mama/Mlezi; ……………………………………………………………………
10. Namba yake ya simu; ………………………………………………………………

## NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI

| NA | JINA | UHUSIANO | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

KIAMBATISHO C

## AHADI YA KUTEKELEZA WAJIBU

- Mimi…………………………………………………………………………. Nakubali nafasi niliyopata katika shule ya sekondari Msamala kuendelea na masomo.
- Nafahamu kuwa ninagharamiwa na Taifa linalothamini kazi na juhudi.
- Naahidi mbele ya Mzazi/Mlezi wangu kuwa nitajitahidi kwa upeo na uwezo wangu kuwa mwanafunzi mwema.
- Ninaahidi kutoshiriki katika mambo yatakayosababisha mwanafunzi kuachishwa shule.
- Naahidi kuwa nitashirikiana na walimu pamoja na wanafunzi wenzangu katika kila jambo lenye manufaa kwa shule na Taifa kwa ujumla.

………………………………………………….

Saini ya Mwanafunzi

Mimi…………………………………………………………………………………………………

Mzazi/Mlezi wa……………………………………………………………………………………….

nimesoma maelekezo yote na kuelewa. Naahidi kwamba nitampatia mahitaji yote kama ilivyoagizwa katika barua. Ripoti na barua zote zinazohusu mtoto wangu ziletwe kwangu kwa anuani;-

………………………………………………………

………………………………………………………

Jina la Mzazi/Mlezi……………………………………………………………………………………

Mtaa………………………………………………………………………………………………

Saini ya mzazi/Mlezi……………………………………………………..

Mwenyekiti wa Mtaa……………………………………………………………………………………

Tarehe…………………………………    Namba ya simu…………………………………………....

